

Kusafisha na nyuma na kuua virusi nyumbani kwako.

Huu ni mwongozo wa jinsi ya kusafisha na kuua virusi kwa kaya ambazo mtu anayeshukiwa kuwa na au aliyethibitishwa kuwa na COVID-19, anakaa.

Kusafisha na kuua virusi kwenye nyuso ngumu



Vaa glavu zinazoweza kutumika mara moja au zinazoweza kutumika tena ambazo zimetengwa kwa kusafisha na kuua virusi vya COVID-19.

Ikiwa nyuso ni chafu, safisha na sabuni au maji ya sabuni kabla ya kutumia dawa ya kuua virusi.



Bleach ya kaya iliyopunguzwa inaweza kutumika kwa kuua virusi.

Tayarisha suluhisho la bleach kwa kuchanganya:

- Vijiko 5 vya chakula (1/3 kikombe) bleach kwa galoni moja ya maji au
- Vijiko 4 vya chai kwa lita moja ya maji.

Kusafisha na kuua virusi kwenye nyuso laini



Nyuso laini, kama sakafu ya mazulia, mazulia madogo nene au mapazia zinapaswa kusafishwa kwa vifaa sahihi vya kusafisha.

Baada ya kusafisha, osha uso laini kama ilivyoelekezwa na mtengenezaji. Tumia mpangilio sahihi wa maji na kausha kabisa.

Vifaa vya Umeme

Hizi ni pamoja na simu za mkononi, kompyuta kibao, skrini za kugusa, vidhibiti vya mbali vya tv na kibodi.



Tumia vifuniko vya vifaa vya umeme vinavyoweza kupanguswa kama unaweza.

Fuata maelekezo ya kusafisha uliyopewa na mtengenezaji. Ikiwa hakuna, tumia vifaa vyenye mchanganyiko wa pombe vya kufutia au kupulizia vilivyo na angalau 70% ya dawa ya kuua, kisha kausha kabisa. Usitumie dawa ya kuua za Clorox.

Kufua nguo

Vitu vya kufua ni pamoja na kitambaa cha kitani, mavazi na vitu vingine



Vaa glavu zinazoweza kutumika mara moja au zinazoweza kutumika tena ambazo zimetengwa kwa kusafisha na kuua virusi vya COVID-19. Ikiwa hutumii glavu, hakikisha umenawa mikono yako mara baada.

Usikung'ute nguo chafu ili kuepuka kutawanywa virusi hewani.

Osha vitu ukitumia mpangilio unaofaa wa maji ya moto na kausha kabisa.

Safisha kikapu cha nguo kwa kutumia dawa ya kuu virusi. Jaribu kutumia mfuko unaotumika mara moja kwenye vikapu vya nguo.

Takataka



Ikiwezekana, jitolee kumpatia mgonjwa pipa la takataka lenye mfuko.

Tumia glavu wakati wa kushughulikia na kuondoa takataka. Nawa mikono yako mara baada ya kumaliza.

Sources:

CDC - <https://www.cdc.gov/coronavirus/2019-nCoV/index.html>

Updated May 26, 2020